JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

015 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda : Saa 3:00 **Mwaka: 2020**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na tatu (13)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **Matatu (3)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **ishirini (20),** sehemu B alama **thelathini na tano (35)** na sehemu C ina alama **arobaini na tano (45)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Scanned with CamScanner

SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. **Katika kipengele (i) – (xv), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.**

(i) **Ipi ni orodha sahihi ya waandishi wa vitabu vya "Sahihi Sitta"?**

A Tirmidhy, Hambali, Ibun majah, Abuu Daud, Muslim na Bukhari
B Muslim, Tirmidhy, Annasai Shaffi, Abuu Daud na Bukhar
C Tirmidhy, Annasai, Ibun majah, Annas bin Malik na Muslim
D Tirmidhy, Annasai, Ibun majah, Abuu Daud, Muslim na Bukhari
E Tirmidhy Annasai, Abu Hurayra, Abuu Daud, Muslim na Bukhari

(ii) **Bainisha vipindi tofauti vya uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w).**

A Uandishi kipindi cha Mtume (s.a.w), Maswahaba, Tabii na Tabii Tabiina.
B Uandishi kipindi cha Abubakar, Umary, Athuman na Ally (r.a).
C Uandishi katika vipindi vya Abu huraira, Bibi Aisha, Abdullah bin Umar (r.a).
D Uandishi katika vipindi vya Rafii, Samrat na Anas bin Malik.
E Uandishi kipindi cha Maswahaba na baada ya maswahaba wote kufa.

(iii) **"Kila jambo jema analolifanya Muislamu ni Sadaka" (Bukhari na Muslim). Kwa mujibu wa sayansi ya Hadithi, Bukhari na Muslim wanasimama katika nafasi gani?**

A Waanzilishi wa Hadithi.
B Waandishi wa Hadithi.
C Wasimulizi wa Hadithi.
D Wadhoofishaji wa Hadithi.
E Wasanifishaji wa Hadithi.

(iv) **Bainisha dhana ya kimapinduzi inayolenga kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye giza la ujahili na ukafiri na kumpeleka katika mwangaza wa uchamungu.**

A Mustalah Al Hadith
B Tarekh
C Tawhiid
D Fiqh
E Sirah

(v) **"Dini ni imani juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu muumba." Ni upi msingi wa upotofu wa tafsiri hii?**

A Imetolewa na makafiri.
B Mungu si lazima awe muumba.
C Haitoshelezi mahitaji.
D Mungu hatambui dini ila Uislamu tu.
E Kwa sababu imetokana na kamusi.

Scanned with CamScanner

(vi) Kwa nini Mwenyezi Mungu alivileta vitabu vya Taurat, Injili, na Zaburi?

A Kuamsha midahalo baina ya wakristo na waislamu.
B Ili Kufundisha watu jinsi ya kusoma na kuandika.
C Kuwapa wanaadamu habari za mambo ya kale.
D Kuwaongoza wanaadamu katika njia iliyonyooka.
E Ili kuanzisha fani mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

(vii) Bainisha tofauti kati ya kuchukua Udhu kwa maji na Kutayammamu.

A Kwa Tayammam mtu haruhusiwi kutufu.
B Tayammam haruhusiwi asiyekuwa mgonjwa.
C Tayammam hairuhusiwi kufanywa na wanawake.
D Kwa kutayammam mtu haruhusiwi kwenda Arafa.
E Tayammam inarudiwa kila inapofika swala nyingine.

(viii) "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano". Kutoeleweka kwa maneno haya ya Mtume (s.a.w), kunathibitishwa na mwenendo upi wa Waislamu?

A kuzipamba ibada zao kwa Sunna nyingi.
B Kuzitekeleza ibada zote na kwa wingi.
C Kutekeleza baadhi ya ibada na kuziacha nyingine.
D Kutekeleza ibada maalumu bila kuzingatia athari zake.
E Kubuni ibada mpya ili kujiongezea uchamungu.

(ix) Nini hukumu ya mtu aliyeacha kufunga siku moja kwa makusudi ?

A Atatakiwa ailipe kadha baada ya Ramadhani.
B Hatoruhusiwa kuendelea kufunga tena siku zitakazobaki.
C Atatoa kafara ya ngamia mmoja na kumwacha huru mtumwa.
D Atafunga miezi miwili mfululizo bila kuacha hata siku moja.
E Hatoweza kuilipa hata kama atafunga mwaka mzima.

(x) Yupi miongoni mwa Maswahaba hawa wa Mtume (s.a.w) ni kati ya waandishi wa Qur'an?

A Uba'y bin Kaab
B Ammar bin Yasir
C Anas bin Malik
D Bilal bin Rabaa
E Ibn Abbas

(xi) Ni ipi tofauti ya msingi baina ya Qur'an na Hadithi?

A Qur'an ina sura nyingi kulinganisha na Hadithi.
B Qur'an imeshuka usiku na Hadithi zimeshuka mchana.
C Qur'an imekuja neno kwa neno na Hadithi imekuja kwa Ilham.
D Qur'an imeshuka katika Swala na Hadithi zimeshuka nyumbani.
E Qur'an kuna Qudusiy na Nabawiy na Hadithi kuna Nabawiy tu.

Scanned with CamScanner

(xii) Jozi ipi inaeleza vema vituo vyote muhimu katika mchakato wa kushuka Qur'an ?

A Lawhim Mahfudh – Wingu wa dunia – Jabal Hira.
B Jabal Hira – Lawhim Mahfudh – Wingu wa Dunia.
C Laylatul Qadr, Lawhim Mahfudh – Jabal Hira.
D Wingu wa Dunia – Lawhim Mahfudh – Jabal Hira.
E Lawhim Mahfudh – Jabal Hira – Wingu wa Dunia.

(xiii) Ni sentensi ipi kati ya zifuatazo inabainisha madai ya Mtume wa uongo Musailama?

A Kumiliki mali zote za dunia kwakuwa wao ndio viongozi wake.
B Kumiliki nusu ya dunia na nusu nyingine ni ya Maqurayshi.
C Kuteremshiwa amri kama ilivyokua kwa Mtume Muhammad (s.a.w).
D Kuumba dunia kwa idhini ya Allah (s.w) Muumba wa binadamu wote.
E Kumuingiza Motoni kila atakayekwenda kinyume na amri ya Allah (s.w).

(xiv) Ishara gani iliyowaongoza maswahaba kumchagua Abu Bakr Swidiq (r.a) kuwa kiongozi wa Dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w)?

A Umashuhuri na mapenzi yake kwa jamii ya Makkah.
B Upole na huruma yake kwa watu wanyonge na masikini.
C Kuteuliwa na Mtume (s.a.w) kuongoza Swala ya jamaa.
D Uchamungu, afya njema na ujuzi wa Qur'an na Sunnah.
E Ukaribu wake na Mtume (s.a.w) na maswahaba wengine.

(xv) Ni sababu ipi kubwa iliyosababisha kuanguka kwa Dola ya Kiislamu aliyoiacha Mtume (s.a.w) ?

A kuwepo kwa harakati za Abdallah bin Sabaa Makka.
B kugombanishwa na washirikina maadui wa Uislamu.
C kugombana Waislamu wenyewe kwa wenyewe.
D Imani dhaifu ya waumini wa dini ya Kiislamu.
E Fitna za Mayahudi na Wakristo wa Madinah.

2. Oanisha tafsiri za ki-Fiqh zilizopo katika **Orodha A** na istilahi zilizopo katika **Orodha B** kama zinavyotumika katika Ibada ya Swala, kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		Orodha B	
(i)	Wito unaoashiria kusimama kwa Ibada ya Swala.	A	Qabliya
(ii)	Sunnah inayoswaliwa baada ya kuchomoza jua na kabla ya mchana.	B	Tashahud
		C	Takbirat Ihram
(iii)	Nguzo ya matamshi katika swala.	D	Mutlaq
(iv)	Kifunguzi cha Ibada ya Swala.	E	Dhuha
(v)	Maji ya asili yanayofaa kujitwaharishia.	F	Iqama
		G	Adhana

Scanned with CamScanner

SEHEMU B (Alama 35)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. Linganisha makosa mawili ya watu wa Nabii Lut na yale yanayofanyika katika zama hizi.

4. Chambua faida mbili unazoweza kuzipata kwa kuanza kila jambo jema kwa Bismillahir Rahmanir Rahiim.

5. Eleza kwa ufupi namna mbili zinazokubalika katika Uislamu kuigawanya elimu.

6. Kwa kutumia jedwali andika hoja tano kutofautisha Zakat ya mali na Zakatul Fitri.

7. (a) Toa maana ya Fiqh.
   (b) Onesha jinsi misingi mitatu ya Fiqh inavyotegemeana.

8. (a) Eleza maana ya Hadithi sahihi.
   (b) Taja vigezo vinne vya Hadithi sahihi kwa kuzingatia Matini yake.

9. "*Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu*"(51:56). Eleza namna ambayo mwanadamu atalitekeleza lengo la kuumbwa kwake.

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii.

10. Bainisha tofauti nne kati ya Funga ya Ramadhani na Funga za Sunnah.

11. Thibitisha kwa kutumia hoja tano kuwa Uislamu unasisitiza utafutaji wa elimu

12. (a) Onesha hatua tatu alizochukuwa Mtume (s.a.w) katika kuihifadhi Qur'an kimaandishi.
    (b) Kwa nini Qur'ani ilinakiliwa upya wakati wa khalifa Uthman (r.a)?

13. Kwa kutumia hoja sita eleza madhara watakayopata Waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya Uislamu.

csee2020

Scanned with CamScanner